

## **Jibu:** Kuapisha kunatokana na Neno “**Apa/ kiapo**”

---

Kwahiyo mtu “**anapoapa**” kwa niaba ya mwingine maana yake  
“**kamwapisha yule mtu**”

Zamani mtu alikuwa anaweza kuapa mwenyewe kwa MUNGU mfano...

Na pia Mtu alikuwa anaweza kumwapisha mwingine, na kiapo kile kikawa na nguvu ile ile kana kwamba mtu yule kaapa kwa nafsi yake, na wala hajaapiwa..mfano ni yule Mtumishi wa Ibrahimu ambaye Ibrahimu alimtuma akamtwalie mke mwanae Isaka, kwamba asimtwalie mtoto wake mke kutoka kwa watu wengine isipokuwa wa nyumbani kwake Ibrahimu.

Kuapisha ni kufanya nini? (Mwanzo 24:2).

*Mwanzo 24:2 "Ibrahimu akamwambia mtumishi wake, mzee wa nyumba yake, aliyetawala vitu vyake vyote, Tafadhali uutie mkono wako chini ya paja langu,*

*3 NAMI NITAKUAPISHA KWA BWANA, Mungu wa mbingu, na Mungu wa nchi, kwamba hutamtalia mwanangu mke katika binti za Wakanaani ambao nakaa kati yao;*

*4 bali enenda hata nchi yangu, na kwa jamaa zangu, ukamtwalie mwanangu Isaka mke*

Tunasoma, yule mtumishi alikichukua kile kiapo kama cha kwake, na alijihadhari asiende kinyume na kiapo kile..

*Mwanzo 24:37 "Kisha bwana wangu akaniapisha akisema, Usimtwalie mwanangu mke wa binti za Wakanaani, ambao nakaa katika nchi yao"*

Utaona pia Yusufu aliwaapisha wana wa Israeli juu ya mifupa yake

Kuapisha ni kufanya nini? (Mwanzo 24:2).

wakati watakapotoka Misri, kwani aliwaambia wasiiache mifupa yake Misri, soma **Mwanzo 50:25 na Kutoka 13:19.**

Zaidi utaona kipindi Makuhani wamemkamata BWANA, walimlazimisha azungumzwe yeye ni nani kwa kumwapisha kwa MUNGU.

*Mathayo 26:62 “Kisha Kuhani Mkuu akasimama akamwambia,  
Hujibu neno? Hawa wanakushuhudia nini?*

*63 Lakini, Yesu akanyamaza. Kuhani Mkuu akamwambia,  
Nakuapisha kwa Mungu aliye hai, utuambie kama wewe ndiwe  
Kristo, Mwana wa Mungu.*

*64 Yesu akamwambia, Wewe umesema; lakini nawaambieni, Tangu  
sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa  
nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni”*

Vile vile utaona pia kuna watu walijaribu kuyaapisha mapepo kwa Bwana yawatoke watu, (*Matendo 19:13*) na pia mapepo nayo yanaonekana kujaribu kumwapisha Bwana YESU (*Marko 5:7*).

Kuapisha ni kufanya nini? (Mwanzo 24:2).

Mistari mingine inayozungumzia kuapishwa kwa mtu/watu ni pamoja na ***Yoshua 6:26, Yoshua 23:7, 1Samweli 14:24, 1Wafalme 18:10, Ezra 10:5 na 1Wathesalonike 5:27.***

Je unaye Mwokozi YESU moyoni mwako?

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

**Mafundisho mengine:**

**[Kutia mkono chini ya paja kama ishara ya kiapo, kulimaanisha](#)**

Kuapisha ni kufanya nini? (Mwanzo 24:2).

**nini?**

## **USIPOTEZWE NA MANENO YA MANABII WA UONGO.**

**Ni vitu vipi hivyo viwili visivyoweza kubadilika? (Ebr 6:18)**

**Nchi ya “Kabuli” ndio nchi gani kwasasa, na kwanini iliitwa  
hivyo? (1Wafalme 9:13).**

**AKIKI NA YASPI NI MADINI GANI?**

**Rudi Nyumbani**

Share on:

WhatsApp

[Print this post](#)